Gharama Kubwa Ya Zawadi Ya Bure

(The High Cost Of A Free Gift)

Na

Ellis P. Forsman

Gharama Kubwa Ya Zawadi Ya Bure

Na

Ellis P. Forsman

Oktoba 15, 2011

Gharama Kubwa Ya Zawadi Ya Bure

Rum. 6:23

Pengine umewahi kusikia wakisema “Vitu vizuri katika maisha ni vya bure!” Hii ni kweli hasa unapoangalia kwamba kitu “kizuri” kaatika maisha ni zawadi.

Ninaongelea kile ambacho Mungu anawapa wote watakao mkubali: “uzima wa milele”. Hakika ni “zaawadi toka kwa Mungu”!

Rum. 6:23, “*Maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu.*”

Alafu, uzima wa milele ni zawadi…

- Gharama kubwa ililipwa ili kutoa zawadi.
- Na gharama kubwa lazima ilipwe ili uwezo kuipokea.

Gharama kubwa kwa zawadi ya bure? Inawezekanaje?

“Mithali” huu wakati mwingine unaweza kuwa mgumu kuelewa.

Hataivyo, mafundisho ya Yesu mara nyingi hupatikana katika mfumo wa “mithali”

Mat. 5:3-6, “*Heri walio maskini war oho maana ufalme wa mbinguni ni wao. Heri wenye huzuni maana hao watafarijika. Heri wenye upole; maana hao watairithi nchi. Heri wenye njaa na kiu ya haki; maana hao watashibishwa.*”

Kwa uchunguzi wa karibu, “mithali” kama hii haichanganyi, bali ni maelezo ya ukweli muhimu wa kiroho!

Katika somo hili, tutaenda kuangalia jinsi zawadi hiyo ya bure inawezaje kuwa yenye gharama, tukianza na:

Zawadi ya bure ya wokovu

Wengi wana dhana mbaya kuhusiana na jinsi wokovu unavyopatikana.

“Mkubali Kristo tu na utaokoka” ndio shauri la wengi.

Na watu wengi wanadhani kwamba ni swala la “kumkubali”, “bila kuwepo na kiunganishi”. Hataivyo, angalia maneno ya Yesu mwenyewe.

Yoh. 14: 21-23, “*Yeye aliye na amri zangu na kuzishika, yeye ndiye anipendaye; naye anipendaye atapendwa na Baba yangu; nami nitampenda na kujidhihirisha kwake. Yuda (siye iskariote), akamwamba Bwana imekuwaje ya kwamba wataka kujidhihirisha kwetu, wala si kwa ulimwengu?*

Yesu akajibu akamwambia, mtu akinipenda atalishika neno langu; na Baba yangu atampenda; nasi tutakuja kwake na kufanya makao kwake."

"Kumpokea Yesu" inahitaji kujisalimisha kwa Ubwana wa Kristo, kukubali maagizo yake.

Yoh. 15:10, "*Mkizishika amri zangu mtakaa katika pendo langu; kaama vile mimi nilivyozishika amri za Baba yangu na kukaa katika pendo lake.*"

Wokovu ni zawadi ya Mungu kwa mwanadamu asiyefaa.

Ilitolewa tulipokuwa tungali wenye dhambi, wasio na mungu, na maadui.

Rum. 5:6-8, "*Kwa maana hapo tulipokuwa hatuna nguvu, wakati ulipotimia, Kristo alikufa kwa ajili yaa waovu. Kwa kuwa ni shidaa mtu kufa kwa ajili ya mtu mwenye haki; lakini yawezekana mtu kuthubutu kufa kwa ajili ya mtu aliye mwema. Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu sisi tulipokuwa tungali wenye dhambi.*"

Siyo kwa sababu tunampenda Mungu, bali kwa sababu alitupenda sisi!

1 Yoh. 4:9-10, "*Katika hili pendo la Mungu lilionekana kwetu, kwamba Mungu amemtuma Mwanawe pekee ulimwenguni ili tupate uzima kwa yeye. Hili ndilo pendo, si kwamba sisi tulimpenda Mungu, bali kwamba yeye alitupenda sisi akamtuma Mwanawe kuwa kipatanisho kwa dhambi zetu.*"

Na inatolewa kwa wote wanaopenda kuipokea!

- Ufu. 21:6, "*Akaniambia imekwisha kuwa. Mimi ni Alfa na Omega, Mwanzo na Mwisho. Mimi nitampa yeye mwenye kiu ya chemchemi ya maji ya uzima bure.*"
- Ufu. 22:17, "*Na Roho na Bibi – arusi wasema njoo! Naye asikiaye na aseme njoo! Naye mwenye kiu na aje; nay eye atakaye, na ayatwae maji ya uzima bure.*"

Alafu, wokovu unatolewa "bure". Je hiyo inamanisha haina gharama yo yote? Siyo!

Hakika, tutaona kwamba hakuna chochote katika ulimwengu wote uliogharimu zaidi.

Gharama kubwa ya kutoa zawadi

Ilichomgharimu Baba.

- Yoh. 3:16, "*Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe pekee ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.*"
- Rum. 8:32, "*Yeye asiyemwachilia Mwana wake mwenyewe, bali alimtoa kwa ajili yetu sisi sote, atakosaje kutukirimia na mambo yote pamoja naye.*"

Ilimgharimu dhabihu ya Mwanaye mpendwa pekee! Hakumuacha Mwanaye katika juhudi za kutuokoa kutoka katika dhambi zetu!

Ilichomgharimu Mwana.

Fil. 2:5-8, "*Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwamo pia ndani ya Kristo Yesu; ambaye yeye mwanzo alikuwa yuna namna ya Mungu naye hakuona kule kuwa sawa na Mungu kuwa ni kitu chaa kushikamana nacho; bali alijifanya kuwa haana utukufu, akatwaa namna ya utumwa, akawa anamfano wa wanadamu; tena alipoonekana ana umbo kama mwanadamu, alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti, naam mauti ya msalaba.*"

Ilimgharimu utukufu na ukuu wa mbingu, aliokuwa nao naa Baba kabla hajaja ulimwenguni hapa.

Ilimgharimu upole wa utumishi, hata katika hatua kuteseka na hatimaye kufa kwa kusulubishwa kwa ajili ya dhambi zetu.

Ilichoigharimu Roho Mtakatifu

- 2 Thes. 2: 13-14, "*Lakini imetupasa sisi kumshukuru Mungu sikuzote kwa ajili yenu, ndugu mliopendwa na Bwana kwa kuwa Mungu amewachagua tangu mwanzo mpate wokovu, katika kutakaswa na Roho, na kuiamini kweli; alivyowaitia ninyi kwa injili yetu ili kuupata utukufu wa Bwana wetu Yesu Kristo.*"
- Efe. 4:30, "*Wala msimhuzunishe yule Roho Mtakatifu wa Mungu; ambaye kwa yeye mlitiwa muhuru hata siku ya ukombozi.*"

Huduma iliyofanywa kwa miongo ya uvumilivu kwa mioyo ya wenye dhambi inayosumbua kupitia wito wa injili.

Akivumilia mateso ya wanadamu waliomtendea ubaya, akihuzunishwa pale walipompinga.

Mungu, Yesu Kristo, na Roho Mtakatifu wamelipia kwa upendo ili kufanya zawadi ya wokovu iwezekane. Hivyo inawezekana kwa mtazamo wa "utoaji", wake tunaweza kuona "Gharama Kubwa Ya Zawadi Ya Bure".

Lakini "kukubali" zawadi hii ya bure inagharama pia.

Gharama kubwa ya kuikubali zawadi

Ina gharama ya kujikana mwenyewe, kwa wanadamu wanaoushikilia sana.

Paulo alilipa gharama kwa furaha, akieleza waziwazi katika vifungu kadhaa.

- Gal. 2:20, "*Nimesulubiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndaani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda akijitoa nafsi yake kwa ajili yangu.*"
- Fil. 3: 7-8, "*Lakini mambo yale yaliyokuwa faida kwangu, naliyahesabu kuwa hasara kwa ajili ya Kristo. Naam, zaidi ya hayo nayahesabu mambo yote kuwa hasara kwa ajili ya uzuri usio na kiasi wa kumjua Kristo Yesu, Bwana wangu; ambaye kwa ajili yake nimepata hasara ya mambo yote nikiyahesabu kuwa kama mavi ili nipate Kristo.*"

Mtu hawezi kumpokea Yesu Kristo na wokovu katika mtazamo mdogo kuliko kujitoa kikamilifu kwake.

Hii inafanya injili ya Kristo “injili ngumu” kwa wengi kuikubali. Wanataaka kumkubali Yesu kama mwokozi, lakini siyo kama Bwana wa maisha yao.

Hata wengine wanasema kuwa kumkubali Yesu kama Mwokozi na kama Bwana ni vitendo viwili tofauti.

Lakini viwili havitenganishwi.

- Luka 2:11, “*Maana leo katika mji wa Daudi amezaliwa kwa ajili yenu, Mwokozi ndiye Kristo Bwana.*”
- Mdo. 2:36, “*Basi nyumba yote ya Israeli na wajue yakini ya kwamba Mungu amemfanya Yesu huyo mliyemsulibisha kuwa Bwana na Kristo.*”
- Mdo. 10:36, “*Neno lile alilowapelekea wana wa Israeli akihubiri habari njema ya amani kwwa Yesu Kristo (ndiye Bwana wa wote),*”

Hayupo mwanadamu anayeweza kumkubali Yesu kama “Mwokozi wa roho yake” bila kumkubali kama “Bwana wa maisha yake”!

Yesu mwenyewe aliliweka hili wazi alipowaonya wasikilizaji wake kwamba gharama ya kuwa mwanafunzi iko juu.

Luka 14:25-33, “*Makutano mengi walipokuwa wakifuata naye aligeuka akawaambia, kama mtu akija kwangu naye hamchukii baba yake, na mama yake, na mke wake, na wanawe, na ndugu zake waume na wake; naam, na hata nafsi yake mwenyewe, hawezi kuwa mwanafunzi wangu. Maana ni nani katika ninyi, kama akitaka kujenga mnara, asiyeketi kwanza na kuhesabu gharama, kwamba anayo vya kuumalizia? Asije akashindwa kuumaliza baada ya kuupiga msingi watu wote waonao wakaanza kumdhihaki, wakisema, mtu huyu alianza kujenga akawa hana nguvu ya kumaliza. Au kuna mfalme gani akitaka kwenda kupigana na mfalme mwingine, asiyeketi kwanza na kufanya shauri, kwamba yeye pamoja na watu elfu kumi ataweza kukuta na yule anayekuja juu yake na watu elfu ishirini? Na kama akiona hawezi hutuma ujumbe kutaka shauri za amani, mtu yule akali mbali. Basi kadhalika kila mmoja wenu asiyeacha vyote alivyo navyo, hawezi kuwa mwanafunzi wangu.*”

Ubwana wa Yesu binafsi, uzima, na umiliki ni lazima ukiri ikiwa tunapaswa kumfaahamu kama Bwana!

Ni lazima watu wafahamu kwamba Yesu aliwaagiza wanafunzi wake kuhubiri “toba na msamaha wa dhambi kwa jina lake”.

Luka 24:47, “*Na kwmba mataifa yote watahubiriwa kwa jina lake habari yaa toba na ondoleo la dhambi, kuanza tangu Yerusalemu.*”

Hakuna msamaha tofauti na toba! Na toba inajumuisha maisha yote!

2 Kor. 7:10-11, “*Maana huzuni iliyo kwa jinsi ya Mungu hufanya toba liletalo wokovu lisilo na majuto; bali huzuni ya dunia hufanya mauti. Maana angalieni kuhuzunishwa huko kwa jinsi ya Mungu kulitenda bidii kama nini ndani yenu; naam, na kujitetea, naam, na kukasirika, naam, na hofu, naam, shauku, naam, na kujitahidi, naam, na kisasi! Kwa akila njia mmejionyesha wenyewe kuwa safi katika jambo hilo.*”

Siyo huzuni ya mambo yaliyopita ndoyo inaongoza katika toba, bali shauku na amasa kwa ajili ya wakati ujao, ndiyo itakayoamua tutakavyoishi.

Toba ni kuacha njia zetu za ubinafsi, ili twende njia ya Mungu katika kutii na kuwa na ushirika pamoja naye.

Hitimisho

Hiyo ndiyo sababu "zawadi" ya wokovu, inapotolewa bure, bado inakuja na gharama ya juu.

Ubwana wa Yesu hakika inahitaji kujitoa kikamilifu katika mamlaka yake.

Mat. 28:18-20, "*Yesu akaja kwao akasema nao, akawaambia, nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari.*"

Ndio, zawadi ya wokovu inagharama.

Ilimgharimu Mungu zaidi ya kile ambacho mbingu inaweza kusema.

Ilimgharimu Yesu maumivu na aibu ya msalaba.

Hata leo inaigharimu Roho Mtakatifu anayetafuta kukuingiza kupitia injili.

Inamgharimu kila mmoja anayepokea kwa haki kujitoa kwa uhakika kwa Yesu na watakaokuwa wake kwa wakati huu na milele!

Yesu amelipa gharama kubwa ili kukupa zawadi ya wokovu.

Mdo. 2:36-39, "*Basi nyumbaa yote ya Israeli na wajue yakini ya kwamba Mungu amemfanya Yesu huyo mliyemsulibisha kuwa Bwana na Kristo. Walipoyasikia haya wakachomwa mioyo yao, wakamwambia Petro na mitume wengine, tutendeje ndugu zetu? Petro akawaambia tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie.*"

Je umelipa gharama kubwa ya kukubali zawadi ya wokovu? Unapaswa kufanyika Mkristo. Zifuatazo ni hatua muhimu za kulifanya hilo liwezekane.

- **Imani.** Waeb. 11:6*, "Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa dhawabu wale wamtafutao."* Nilipokuwa shuleni (nikiwa na miaka 17), kijana mmoja jirani yangu mwaka sawa na mimi akniambia kwamba haamini kwamba Mungu yuko. Kwa vile nilisha batizwa, nilichukua nafasi ya kuongea naye kuhusu mandiko. Akaniambia kwamba anaweza kuona kwamba kuishi maisha ya ukristo ni nzuri, lakini hakuwa na uhakika kwamba Mungu yuko. Lakini ili kuwa upande salama, labda anapaswa kwenda kanisani,

na akifa na kusimama mbele za Mungu (kama kuna Mungu) siku ya hukumu (kama kuna hukumu), labda kama Mungu akiona kuwa amekwenda kanisani atampeleka mbinguni (kama kuna mbingu), na si motoni (kama kuna moto). Nikamwambia, "haifanyi kazi kwa njia hiyo. Lazima uamini katika yeye kwa moyo wako wote la sivyo huwezi kumpendeza.

- **Toba.** Matend. 2:38*, "Petro akawambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina lake Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi zenu nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."*

Matend 11:18*, ".....Basi Mungu amewajalia hata mataifa nao <u>toba liletalo uzima."</u>*

Kama ulikuwa unalala, ukasikia kelele kwenye chumba kingine, na unafikiria mwenyewe, "Kwamba kuna mwizi!" taratibu unachukua simu ya mkononi, unawapigia polisi. Kidogo polisi wanafika na kumshika mwizi. Alafu anapiga kelele, "samahani; samahani!" Anaomba msamaha wa nini? Kwa sababu amekamatwa; si kwamba ameiba. Toba iliyokweli ni kwamba mwizi angeomba msamaha kwamba hataiba tena. Hiyo ndio toba ya kweli. Ni badiliko la nia linaloleta badiliko la matendo. Tunatakiwa kufanya hivyo kabla hatujawa wakristo.

- **Kukiri.** Waru. 10:9-10*, "Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana <u>kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu."</u>*

Tuna kiri nini? Kwamba tuna amini kwamba Yesu Kristo ni mwana wa Mungu.

Kumbuka kwamba katika andiko hilo hapo juu kwamba imani (kuamini), toba, na kukiri ni "**KATIKA**" haki, uzima, au wokovu. "Katika" inamanisha kuelekeza kwenye kitu Fulani; si kwamba mtu ameshapata.

- **Ubatizo.** Ni katika ubatizo ndipo haki, uzima, na wokovu vinapatikana. Yesu mwenyewe alibatizwa kuitimiza haki yote*, "Lakini Yohana alitaka kumzuia akisema, mimi nahitaji kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu? Yesu akajibu akamwambia kubali hivi sasa, kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote. Basi akamkubali. Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini, na tazama mbingu zikamfunukia akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua, akija juu yake; na tazama sauti kutoka mbinguni ikisema, huyu ni mwanangu mpendwa, ninaye pendezwa naye."* (Math. 3:14-17). Yesu alibatizwa kwa sababu Mungu alisema ni jambo sahihi la kufanya. Unaona ni jinsi gani ilivyompendeza Mungu Yesu alipobatizwa? Yesu pia akasema, "*Imekuwa kwetu <u>**sisi**</u> kuitimiza haki yote."* Tuna batizwa kwa sababu inatimiza haki yake yote, si kwa sababu ni haki yetu.

Kwa kweli, tusipo batizwa, tungali katika dhambi zetu. *"Petro akawambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina lake Yesu Kristo <u>kwa ajili ya ondoleo la dhambi</u>, na*

mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu." (Matend. 2:38). Petro, umesema kusudi la ubatizo ni nini? "*Kwa ajili ya ondoleo la dhambi*". Kwa nini watu wanapenda kuach hatua inayotuondoa dhambi zetu?

Yesu aliamuru kwamba ili kuufikia wokovu lazima tubatizwe. *"Na akawambia enendeni ulimwenguni kote mkahubiri injili kwa kila kiumbe. Aaminiye **na** kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa."* (Marko 16:15-16).

Anania alimwambia Sauli (kabla hajaitwa Paulo) kitu iki hiki, "*Unakawilia nini? Simama, na ubatizwe, na uoshwe dhambi zako, ukiliitia jina la Bwana."* (Matend. 22:16). Ubatizo ni hitaji lililotolewa na Mungu.

Ubatizo unaitwa maziko, *"Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima."* (Waru. 6:4). Utu wetu wa kale umekufa. *"Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake. Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima. Kwa maana kama mlvyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika mtaunganika katika mfano wa kufufuka kwake; mkijua neno hili ya kuwa utuwetu wa kale ulisulubishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusiitumikie dhambi tena."* (Waru. 6:3-6). Ubatizo ni ramani ya Mungu inayotumiwa na damu ya Kristo katika maisha yetu kwa ubatizo. Tunakuwa huru na dhambi zetu za zamani kama tu tukibatizwa.

Hii haimanishi "kunyunyiza. Andiko hilo hapo juu linasema ubatizo ni maziko. Hatuwezi kupeleka maiti makaburini, na kumwekea udongo kidogo juu yake; tunazika mwili.

Kama hujafanyika Mkristo, kwa nini usizingatie leo?